

## HALMASHAURI YA WILAYA PANGANI



### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI FEBRUARI, 2018

#### UTANGULIZI Mh Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri imepanga kutekeleza bajeti yake yenye jumla ya **Shilingi 14,515,222,926/-** zinazotarajiwa kukusanywa katika vyanzo mbalimbali ikiwemo makusanyo ya ndani, ruzuku kutoka serikali kuu pamoja na ruzuku kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani.

Kiasi hicho cha fedha pia kimepangwa kutumika kugharamia matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara ya watumishi, kugharamia miradi ya maendeleo katika maeneo yote ya wilaya ya Pangani na matumizi mengineyo.

#### 1. MAPATO Mh Mwenyekiti

Katika kipindi cha kufikia mwezi Februari 2018, Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya shilingi **813,080,421.69** na pia kufanya jumla ya mapato yote yaliyokusanywa katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari 2018 kufikia shs **7,685,159,974.17** na kufikia asilimia **53** ya makisio ya mwaka kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama jedwali namba 1 linavyoonyesha hapa chini.

#### Jedwali Na. 1: Mapato ya Mwezi Februari, 2018

N a	CHANZO CHA MAPATO	MAKISIO MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MAPATO HADI JANUARI, 2017	MAPATO MWEZI FEBRUARI, 2017	JUMLA YA MAPATO HADI FEBRUARI, 2018	MAPATO PUNGUFU/ZAIDI	AS ILI MI A
1	Mapato ya ndani	1,290,012,426	562,674,526	104,610,607	667,285,133	(622,727,293)	52
2	Mishahara	9,736,902,500	4,639,038,500	696,476,715	5,335,515,215	(4,401,387,285)	55
3	Mapato ya ruzuku ya matumizi ya kawaida	743,696,965	265,006,800	7,112,000	272,118,800	(471,578,165)	37
4	Mapato ya ruzuku ya miradi	2,706,230,013	1,405,359,726	4,881,100	1,410,240,826	(1,295,989,187)	52
	<b>JUMLA</b>	<b>14,476,841,904</b>	<b>6,872,079,552</b>	<b>813,080,422</b>	<b>7,685,159,974</b>	<b>(6,791,681,929)</b>	<b>53</b>

## 2. MATUMIZI

### Mh Mwenyekiti,

Katika kipindi cha mwezi Februari 2018, jumla ya Shilingi **804,575,079** zimetumika na kufanya matumizi kufikia asilimia **48** ya makisio ya mwaka, kiasi hiki kimetumika katika vyanzo mbalimbali kama jedwali namba 2 linavyoonyesha hapa chini.

### Jedwali Na. 2: Matumizi ya mwezi Februari 2018

N A	CHANZO CHA MATUMIZI	MAKISIO MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MATUMIZI HADI JANUARI,2017	MATUMIZI MWEZI FEBRUARI, 2018	JUMLA YA MATUMIZI HADI FEBRUARI, 2018	MATUMIZI PUNGUFU/ZAI DI	ASILIMIA
1	Mapato ya ndani	1,290,012,426	479,860,230	45,134,730	524,994,960	765,017,466	41
2	Mishahara	9,736,902,500	4,641,534,500	696,476,715	5,335,515,215	4,398,891,285	55
3	Mapato ya ruzuku ya kawaida	743,696,965	226,615,322	42,971,434	269,586,756	474,110,209	36
4	Mapato ya ruzuku ya miradi	2,706,230,013	768,640,589	19,992,200	788,632,789	1,917,597,224	29
	<b>JUMLA</b>	<b>14,476,841,904</b>	<b>6,116,650,641</b>	<b>804,575,079</b>	<b>6,918,729,720</b>	<b>7,555,616,184</b>	<b>48</b>

## MAFANIKIO

### Mh Mwenyekiti,

Makusanyo ya vyanzo vya ndani pekee ni jumla ya **Shilingi 667,285,133** sawa na **asilimia 52**. Mapato haya yamechangiwa na baadhi ya vyanzo vya mapato kufanya vizuri kwa zaidi ya asilimia **67** iliyopaswa kufikiwa mwezi Februari, 2018 kwa lengo la kiasi cha **Shilingi 860,008,284**

Vyanzo hivyo ni kama ifuatavyo:-

- Leseni za biashara Sh. 31,445,286/- sawa na asilimia 90
- Ada ya ukaguzi wa wanyama Sh. 2,638,750/- sawa na asilimia 88
- Ada ya Machijio ya wanyama Sh. 2,300,360/ - sawa na asilimia 92
- Ushuru wa mazao ya bahari Sh. 142,152,805/- sawa na asilimia 97
- NHIF/NSSF Sh. 300,488,267/- sawa na asilimia 82

## **CHANGAMOTO**

### **Mh Mwenyekiti**

- ✓ Upungufu wa wakusanyaji wa mapato ya ndani
- ✓ Kutozingatiwa kwa sheria ndogondogo katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kunapelekea kupungua kwa mapato
- ✓ Kushuka kwa morali ya wakusanyaji kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo motisha
- ✓ Baadhi ya vyanzo vyenye bajeti kubwa kurudishwa serikali kuu kumepelekea kupungua kwa mapato. Mfano; kodi ya majengo na kodi za mabango

## **MIKAKATI**

### **Mhmwenyekiti**

- Kudhibiti gari la kukusanyia mapato liwe linafanya kazi hiyo tu labda ikitokea dharura ndio litumike kwa kazi nyingine
- Kupitia ofisi ya Mwanasheria wa Halmashauri, sheria ndogo zitafikia mwisho wa kuthibitishwa na kurudishwa kwa ajili ya kuzifanyia kazi
- Kuboresha sheria ndogo kila panapo hitajika kufanya hivyo ili ziendane na wakati
- Ni muhimu sasa kuangalia upya motisha kwa wakusanyaji na pia marejesho ya vijiji yapelekwe kwa wakati
- Bajeti lazima iwe na uhalisia na imara kusiwepo na mabadiliko ya sheria za kukusanyia mapato katikati ya utekelezaji wa bajeti za mwaka.

Mchanganuo wa mapato yote na matumizi ya Halmashauri umeonyeshwa kwenye majedwali yaliyoambatanishwa na taarifa hii.

Naomba kuwasilisha.

.....  
**MZEE A. SALIMU**  
**KAIMU MWEKA HAZINA (W)**  
**PANGANI**